



U.S. Department of State
Bureau of International Narcotics
and Law Enforcement Affairs (INL)



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JAJI MKUU AFUNGUA WARSHA YA KUJADILI UHALIFU WA KIMATAIFA ULIO PANGWA

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma amefungua warsha ya wadau wa haki jinai kwa ajili ya kujadiliana nafasi ya sheria katika kupambana na makosa ya Uhalifu wa kupangwa wa kuvuka mipaka yakiwemo ya biashara haramu ya kusafirisha binadamu, dawa za kulevya, uhalifu mitandaoni na uhalifu unaofanana na huo.

Mhe. Prof. Juma amefungua warsha hiyo leo tarehe 03/09/2024 katika Hoteli ya White Sands Resort jijini Dar es Salaam ambao umewaleta pamoja wadau zaidi ya 80 wakiwemo Majaji wa Mahakama kuu, Mahakimu wakazi wakuu, Waendesha Mashtaka, Wataalamu na Wawakilishi mbalimbali wa vyombo vya usimamizi wa sheria, Taasisi za kifedh kutoka Tanzania, Msumbiji na Kenya.

Vyombo hivyo vya usimamizi wa sheria na Taasisi za Umma ni mamlaka za kupambana na dawa za kulevya, uhalifu mitandaoni, uchunguzi wa jinai wa kimaabara, Benki kuu ya Tanzania, Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), TCRA na Jumuiya ya Mabenki Tanzania.

Warsha hiyo imeandaliwa na kuendesha na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya sheria ya Maendeleo (IDLO) na itadumu kwa siku mbili hadi tarehe 04/09/2024.

Katika warsha hiyo wadau hao watajadiliana jinsi ya kuimarisha ushirikiano na ushirikishwaji miongoni mwao katika ngazi za kitaifa na kikanda, na pia kutafakari juu ya kubadilishana taarifa, uzoefu, changamoto, na mbinu bora za kukabiliana na Uhalifu wa Kimataifa uliopangwa miongoni mwa nchi hizo tatu.

Aidha, warsha hiyo inalenga kutafakari na kupitia mapendekezo yanayotokana na Kongamano la wadau wa Mahakama la kujadili makosa ya uhalifu wa kifedha lililofanyika Januari 2024 jijini Dodoma ambalo liliwapa wadau zana na maarifa muhimu ili kukabiliana kwa ufanisi dhidi ya Uhalifu huo wa Kimataifa uliyopangwa.

Imetolewa na Kitengo cha Masoko na Mawasiliano

03/09/2024